Mzabibu Na Matawi

(The Vine And The Branches)

na

Ellis P. Forsman

Mzabibu Na Matawi

(The Vine And The Branches)

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Mzabibu Na Matawi

Yohana 15:1-6

Moja ya anguko kubwa la mwanadamu katika kujifunza Biblia ni kuruhusu tafsiri na mapokeo yaw engine kumvutia katika hitimisho na kuondoa. Kifungu chetu katika somo letu imeteseka vya kutosha au labda zaidi ya kifungu kingine katika Biblia kwa sababu ya kutafsiriwa kimakosa na wanadamu.

Ni makosa yaliyozoeleka, nimesikia mara nyingi kutoka kwa viongozi na washiriki wa madhehebu ya dini tofauti wakisema kwamba madhehebu ya dini zote ni matawi ya kanisa. Wanahitimisha kwamba kanisa la Kristo, katika hali ya ujumla, ni mzabibu na madhehebu mengine yote ni matawi. Huu ni hitimisho wa kimakosa na sio wa kimaandiko. Kwa ukweli eebu tuzingatie kifungu cha maandiko.

Yohana 15:1-6, "*Mimi ndimi mzabibu wa kweli, na Baba yangu ndiye mkulima. Kila tawi ndani yangu lisilozaa huliondoa; na kila tawi lizaalo hulisafisha ili lizidi kuzaa. Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia. Kaeni ndani yaangu, nami ndani yanu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi msipokaa ndani yangu. Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote. Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea.*"

Matawi madhehebu tofauti?

Kusema kwamba matawi ni madhehebu mengi ya dini ni kupotosha kabisa na kufuta mafundisho rahisi ya Yesu. Haiwezekani matawi yakaongelewa kwa madhehebu ya leo kwa sababu tofauti.

Itaonekana kwamba Yesu aliongea kwa wakati uliopo, akiongelea ukweli, au mazingira, ya uwepo bassi. Hii ilikuwa ni miaka mamia kabla ya madhehebu ya kisasa ya siku zetu, ambayo inaweza kudai kuwa mzabibu wa tawi. Hata hawakuwepo wakati ule.

Kuwa ndaani ya Kristo ni kuwa katika kanisa lake, na kanisa lake ssiyo dhehebu, au tawi la dhehebu. Wale wanao okolewa kwa damu ya Kristo ndio wale walio washirika wa kanisa la Bwana.

Mdo. 20:28, "*Jitunzeni nafsi zenu na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe.*"

Wale walio washiriki wa kanisa la Bwana ni wale waliopata ondoleo la dhambi kwa damu ya Kristo, walipotubu na kubatizwa. Kwa umakini zingatia neno la Mungu katika Mdo. 2:38, 41, na 47, "*Petro akwaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. …Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu. …Wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.*"

Katika Heb. 9:22, mtume alitangaza kwamba "*…na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo.*"; hivyo basi, wale wanaotubu na kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi waliokolewa kwa damu ya Kristo, walinunuliwa kwa damu ya Kristo, wakazidishwa katika kanisa la Bwana. kanisa la Kristo haikuwa na siyo dhehebu; vilevile madhehebu hayakuwa na siyo matawi ya kanisa la Kristo.

Kristo hakutumia mifano mibaya kuelezea jambo au kufundishia ukweli. Kitu kimoja ni kweli: inajulikana na ni ukweli unaokubalika, kwamba ni kinyume cha asili na akili ya kawaida kuacha kwamba zabibu mmoja ungeweza kuzaa matawi mia sita tofauti kwa utambuzi tofauti. Unaweza kuona tawi la zabibu ikizaa uzao wa mzabibu, peasi, maharagwe, kunde, tikiti, viazi, na stroberi? Yeyote aliyesikia moja kati ya hizo? Alafu, watu wenye akili nyingi wanaambiwa kuamini kwamba mzabibu mmoja ndio kanisa la Kristo na madhehebu yote tofauti ni matawi. Hitimisho kama hilo siyo ya kufikiria, kwa asili, na kwa neno la Mungu!

Kristo: Mzabibu; Wakristo mmoja mmoja: matawi

Katika kusoma kifungu hiki, itagundulika kwamba Yesu hakutumia kiwakilishi nomino kinacho shabihiana, bali ya kibinafsi. Alisema, "*Mimi ni mzabibu."* Yesu alitangaza kwamba yeye ndio mzabibu, na siyo taasisi ya kidini. Akaendelea kusema, "*Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi msipokaa ndani yangu. Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi.*" Zaidi saana, Bwana wetu alisema, "*Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka.*" Yesu alisema, "**mtu**", binafsi, siyo dhehebu. Mara nyingi, Yesu alikuwa akiongea na mitume wake, na siyo kundi la dhehebu. Akajitolea mfano mwenyewe kama zabibu na kila mtume wake mmoja mmoja kama matawi.

Tofauti na Kristo, hakuna

Siyo tu kwamba Yesu alisema kwamba yeye ni mzabibu na mitume wake matawi, lakini pia alisema, "*pasipo mimi hamwezi kufanya lolote*". Hakika, tawi haliwezi kuwepo pasipo mzabibu. Zaidi sana, jani lazima liwe ndani yaa zabibu ili liweze kuzaa matunda; la sivyo, matawi huchomwa.

Fundisho la Kristo lina thibitisha kwamba tofauti na Kristo mtu hawezi kuwa na tumaini la wokovu. Wanadamu siyo wazuri sana kuweza kujiokoa wenyewe. Hayupo mtu anaweza kupata wokovu tofauti na Kristo. Madhehebu yalitokana na wanadamu, hatakam wanaweza kuwa kidini kivipi, haijalishi wanajaribu kuwa wema kiasi gani, hawana thamani kulingana na jinsi wokovu wa mwanadamu unavyotakiwa. Haijalishi kuhusu kazi yao katika dunia, au kanuni walizopatikana.

Ni majuto kwamba baadhi ya watu hujipa kiburi wenyewe katika ukweli kwamba wanasshikilia ushirika katika dhehebu, kana kwamba ushirika huo unawapatia tiketi ya mbinguni.

Wokovu uko katika Kristo Yesu, kama tunavyoona katika Mdo. 4:12, "*Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.*" Ukombozi na msamaha wa dhambi ziko katika Yesu Kristo.

Mwili mmoja. Efe. 4:4, "*Mwili mmoja na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu.*"

Mwili = kanisa. Kol. 1:18, "*Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote.*"

Kwa vile, kuna kanisa moja. Hakuna wokovu katika kanisa lingine.

Kuvaa jina la Kristo hakulifanyi kundi kuwa washirika wa Kristo. Kwa mfano: Becky, mke wa kaka yangu Evart, siyo mke wangu lakini hataivyo anatumia jina la mwisho linalofanana na langu.

Baraka zote za kiroho zipo katika Yesu Kristo (au katika kanisa lake), kama tunavyoona katika Efe. 1:3-7, "*Atukuzwe Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu war oho ndani yake Kristo; kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu watu wasio na hatia mbele zake katika pendo. Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake. Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha katika huyo Mpendwa. Katika yeye huyo kwa damu*

yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake."

Jinsi tawi lilivyo ndani ya zabibu

Kwa vile mtu hawezi kufanya chochote nje ya Kristo, mtu anaingiaje ndani ya Kristo? Au, tawi linakuwaje sehemu ya zabibu? Jibu ni chanya! Angalia maneno yaliyovuviwa ya mtume Paulo katika Gal. 3:26-27, "*Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*" Swali muhim ni: Waumini wangapi walio katika Kristo? Mrume alisema, "*Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*" Wangapi? Nyote "*…mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*" Muumini aliyetubu "*anabatizwa katika Kristo*", mzabibu wa kweli, alipo na maaisha ya kiroho, ukombozi, msamaha, wokovu! Yesu alisema katika Marko 16:16, "*Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*" Nje ya Kristo, wanadamu wanapotea kwa umilele! "*… Pasipo mimi hamwezi lolote*" kuweza kuokolewa, Kristo alisema. Tawi lazima liwe ndani ya zabibu. Isipokuwa moja iko ndani ya Kristo, kama muumini amebatizwa katika yeye, au hayuko katika Kristo!

Matawi yanaweza kukatwa, potea

Mfano huu mkuu unafundisha kwa mvuto umuhimu wa kuendelea kukaa katika Kristo, mzabibu wa kweli. Yohana 15:3-6, "*Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia. Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi msipokaa ndani yangu. Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote. Mtu asipokaa ndani yangu hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea.*"

Zaidi ya kivuli chochote cha mashaka, Bwana anafundisha kwamba inawezekana mtu akaacha kuwa ndani ya Kristo na akashindwwa kuzaa matunda, hivyo basi, akapoteza nafsi yake katika milele. "*Mtu asipokaa ndani yangu hutupwa nje …",* alisema Yesu. Kama tawi lililokufa lisiloweza kuza, mwanafunzi asiyezaa hukatwa, na kutupwa, na kama tawi, hukusanywa na "*kuchomwa moto*". Hakuna shaka kwa kile kinachoweza kutokea kwa mtu asiyezaa matunda ndani ya Kristo. Kimsingi, Yesu analinganisha, onyo, "*…hukusanywa na kutupwa motoni, na kuchomwa.*" Nyakati za mwisho mkusanyiko na matawi yote yasiyozaa zitahukumiwa.

Luka 18:7-8, "*Na Mungu je hatawapatia haki wateule wake wanaomlilia mchana na usiku, naye ni mvumilivu kwao? Nawaambia atawapatia haki upesi; walakini atakapo kuja Mwana wa Adamu, je! Ataiona imani duniani?*"

Kaamusi ya Coffman: "… kanisa, kwa wakati huo wa mwisho, litapungua na kuwa dogo kwa watakaosalia …"

~ 4000 B.C. Mwanzo wa kipindi cha mababu.

~2000 B.C. Ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu.

30 A.D. Siku ya Pentekoste – Kanisa likaanzishwa.

Akiongelea mwisho wa dunia, Yesu alionyaa katika Mat. 13:41-42, "*Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote na hao watendao maasi, na kuwatupa katika tanuru ya moto, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.*"

Mkutano utakuwa nje ya ufalme wa Bwana, wale waliobatizwa. Kwa Nikodemo, Kristo alisema katika Yohana 3:3-5, "*Yesu akajibu akamwambia, Amin, amin, nakuambia mtu asipozaliwa kwa mara ya pili hawezi kuuona ufalme wa Mungu. Nikodemo akamwambia, awezaje mtu kuzaliwa akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa? Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.*"

Kwa vile hakuna mtu aliye katika ufalme wa Mungu ambaye hajazaliwa kwa mara ya pili, na kwa vile malaika watawakusanya wale waote walio nje ya ufalme wale wote watendao maovu na kuwatupa motoni, inawezekana kwamba baadhi ya wana wa Mungu, wenyeji wa ufalme wake, matawi katika mzabibu wa kweli, Yesu Kristo, watatupwa na watachomwa katika moto wa milele.

Mtume Paulo aliandika kwa ndugu wa Waebrania katika Heb. 6:4-6 kuhusu hatima ya wale watakao anguka, na kushindwa kutubu, na kuendelea kuzaa miba na maguu ya maisha, "*Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionjaa kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, na kulionja neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo, wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsulubisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri.*" Katika msitari wa 8 hitimisho ni, "*Bali ikitoa miiba na magugu hukataliwa na kuwa karibu na laana; ambayo mwisho wake ni kuteketezwa.*"

Kwa ugumu tangazo linaweza kuwa dhahiri.

Wale waangukao na hawatubu na wanazaa matunda ya haki watakataliwa na kuchomwa!

Mtume Paulo alihimiza katika 1 Kor. 9:27, "*Bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe; nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa.*"

Mtume Petro alionya katika 2 Pet. 2:21-22 ya uwezekano wa madhara madhubuti ya kuanguka. Ichukue kwa maana ya hali ya juu, "*Maana ingekuwa heri kwao kama wasingaliijua njia ya haki, kuliko kuijua kisha kuiacha ile amri takatifu waliopewa. Lakini imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli, mbwa ameyarudia maatapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaagaa matopeni.*"